Government of **Western Australia**
Department of **Health**
**Public and Aboriginal Health Division**

# Mpango wa Chanjo wa Mwaka wa 10 Shuleni – taarifa kwa wazazi

## Homa ya uti wa mgongo ni nini?

Ugonjwa wa Meningococcal sio wa kawaida, lakini wakati fulani ni ugonjwa unaohatarisha maisha. Ugonjwa huo ni matokeo ya maambukizi ya bakteria kwenye damu na/au utando unaozunguka uti wa mgongo na ubongo.

Ingawa unatibika kwa viua vijasumu, maambukizi yanaweza kuendelea haraka sana, hivyo ni muhimu kwamba mtu yeyote anayepata dalili za homa ya uti wa mgongo atafute matibabu haraka.

Wakati wowote, takriban asilimia 10 ya watu wenye afya nzuri hubeba bakteria wa homa ya uti wa mgongo bila madhara kwenye pua zao au koo, na hawaugui.

## Homa ya uti wa mgongo inaeneaje?

Bakteria wa homa ya uti wa mgongo huenezwa kwa njia ya hewa (kukohoa, kupiga chafya au busu). Bakteria hawaishi zaidi ya sekunde chache katika mazingira.

Kuna uwezekano mkubwa kwa ugonjwa huo kuenezwa kwa watu wa karibu sana, kama vile watu wanaoishi katika nyumba moja, kukutana kimapenzi na watoto wanaohudhuria huduma moja ya malezi kwa zaidi ya saa nne mfululizo.

## Kwa nini Idara ya Afya ya Australia Magharibi (WA Health) inatoa mpango wa chanjo kwa wanafunzi wenye umri wa Miaka 10?

Homa ya uti wa mgongo inaweza kuathiri kundirika lolote. Hata hivyo, baadhi ya viwango vya juu zaidi vya waenezaji wa homa ya uti wa mgongo na ugonjwa hutokea miongoni mwa vijana wadogo na kundi rika hili linaweza kusambaza bakteria kwa watu walio katika hatari kubwa ya kupata maambukizi, ikiwemo watoto wadogo.

Ni matumaini kwamba kuwachanja wanafunzi wenye umri wa Miaka 10 kutapunguza maambukizi ya bakteria kwa watu wengine na kusaidia kuzuia maambukizi ndani ya jamii kubwa.

## Je, ninahitaji kufanya nini ili kuhakikisha mtoto wangu anapata chanjo?

Kama mzazi/mlezi, unatakiwa kutoa idhini kupitia:

Jukwaa la VaccinateWA la mtandaoni (vaccinatewa.health.wa.gov.au)*

au

Kwa kuchapisha fomu katika healthywa.wa.gov.au/schoolimmunisations na kuirejesha shuleni

*Chaguo halipatikani kwa shule ndani ya Jiji la Joondalup na Visiwa ya Krismasi na Cocos.

## Je, chanjo gani itatumika na ina ufanisi kiasi gani?

Chanjo ya homa ya Uti wa Mgongo ya ACWY itatumika. Chanjo hii inakulinda dhidi ya kundi la vijidudu vinne vya bakteria wa homa ya uti wa mgongo: A, C, W na Y. Chapa ya chanjo Nimenrix® itatumika katika mpango huu wa shuleni.

Chanjo hizi ni salama na madhubuti. Mipango ya chanjo ya homa ya Uti wa Mgongo za ACWY zimetekelezwa kwa vijana wenye umri wa miaka 13 hadi 15 nchini Uingereza tangu 2015 na vijana wenye umri wa miaka 11 hadi 12 nchini Marekani tangu 2005 bila tatizo kubwa kuripotiwa. Chanjo hii mara nyingi hutolewa kama dozi moja. Dozi zaidi zinapendekezwa kwa wale ambao wapo katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa huu na wale ambao wanasafiri kwenda kwenye maeneo ambayo ugonjwa huu upo sana. Tafiti zimeonyesha kwamba ufanisi wa chanjo ya uti wa mgongo ya ACWY ni kati ya asilimia 80–85 kwa vijana wadogo.

## Nani hapaswi kuchanjwa chanjo hii?

Mwambie mtu anayekupa chanjo ikiwa:

- **una mizio mikali, inayotishia maisha.**
  Ikiwa umekuwa na tatizo la mzio linalohatarisha maisha baada ya kupata dozi ya awali ya chanjo ya homa ya uti wa mgongo ya ACWY, au kama una mzio mkali wa viambata vyovyote vya chanjo hii, hupaswi kuchanjwa chanjo hii. Mtoa huduma wako anaweza kukuambia kuhusu viambata vya chanjo.
- **una ujauzito au unanyonyesha.**
  Chanjo za homa ya uti wa mgongo mara nyingi haishauriwi kutolewa kwa wanawake wajawazito au wanaonyonyesha lakini wanaweza kuchanjwa pale inapoonyeshwa kitabibu. Tafadhali jadili zaidi na Daktari wako kama una ujauzito au unanyonyesha.

## Maudhi ya dawa ya dawa ni yapi?

Kama ilivyo kwa dawa yoyote, ikiwemo chanjo, kuna uwezekano wa kutokea maudhi ya kawaida. Kwa kawaida huwa ya wastani na huisha yenyewe. Athari mbaya hutokea pia, lakini ni nadra. Kuna uwezekano mdogo sana wa chanjo kusababisha majera makubwa au kifo. Huwezi kupata maambukizi ya homa ya uti wa mgongo kutokana na chanjo.

Matokeo mabaya ya kawaida ni pamoja na maumivu, uwekundu na uvimbe kwenye sehemu iliyodungwa sindano, homa, kuwashwa, usingizi, kupungua hamu ya kula, maumivu ya kichwa, upele na kichefuchefu. Hata hivyo, athari mbaya ni nadra kutokea.

Chanjo zinakaguliwa kila mara ili kuhakikisha kwamba ni salama na madhubuti. Kupata taarifa kuhusu usalama na maudhi ya kawaida na nadra ya chanjo, tafadhali soma zaidi kwenye: healthywa.wa.gov/immunisation

HealthyWA
healthywa.wa.gov.au

Hati hii inaweza kupatikana katika miundo mingine kama ikiombwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

## Itakuwaje kama athari mbaya itatokea – niangalie nini?

Angalia kitu chochote ambacho kinakuhusu, kama vile dalili za mzio mkali, homa kali, au tabia isiyo ya kawaida. Dalili za mzio mkali zinaweza kujumuisha mabaka kwenye ngozi, kuvimba uso na koo, kupumua kwa shida, mapigo ya moyo kwenda mbio, kizunguzungu, na udhaifu – kwa kawaida ndani ya dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo. Kwa athari yoyote mbaya, wapigie simu ambulensi au nenda kwenye idara ya dharura iliyo karibu nawe.

## Nifanye nini?

Paracetamol inaweza kukusaidia kupunguza homa au maumivu kidogo na kitambaa chenye unyevunyevu pia kinaweza kupunguza maumivu kwenye sehemu iliyodungwa sindano. Tafadhali pata ushauri wa daktari au nenda kwenye idara ya dharura ya eneo lako ikiwa una maudhi yoyote ambayo unadhani ni makubwa au yasiyotarajiwa.

Au piga simu ***healthdirect Australia*** kwa namba 1800 022 222.

Watoa huduma ya chanjo wote Australia Magharibi wanatakiwa na sheria kuripoti athari yoyote mbaya inayosababishwa na chanjo. Wazazi pia wanaweza kutoa taarifa kuhusu masuala yanayohusu athari mbaya inayotokea baada ya chanjo. Pata taarifa zaidi kwenye healthywa.wa.gov.au/WAVSS au piga simu 6456 0208.

## Mawasiliano

**Daktari wa eneo lako, mfamasia, kituo cha afya cha jamii, hospitali au kitengo cha afya ya umma**
healthywa.wa.gov.au/publichealthunits

**healthdirect Australia**
Simu: 1800 022 222

## Taarifa zaidi

**Idara ya Afya**
healthywa.wa.gov.au/immunisation

**Idara ya Afya ya Jumuiya ya Madola**
1800 671 811 au
health.gov.au/health-topics/immunisation

Imetolewa na Kurugenzi ya Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza
© Department of Health 2024

Hakimiliki ya nyenzo hii iko mikononi mwa Jimbo la Australia Magharibi isipokuwa kama imeonyeshwa vinginevyo. Mbali na shughuli yoyote inayofaa kwa madhumuni ya utafiti binafsi, utafiti, ukosoaji au mapitio, kama inavyoruhusiwa kwa mujibu wa kifungu cha *Sheria ya Hakimiliki ya 1968*, hairuhusiwi kunakiliwa au kutumiwa tena andiko hili kwa madhumuni yoyote bila idhini ya maandishi ya Jimbo la Australia Magharibi.

IMM-013356 JAN'23